# Maelekezo ya Udereva kwa lugha ya Kiswahili kutokana na sheria za jimbo la Virginia, USA 2017

Tumia pamoja na kitabu cha Virginia Driver's Manual – Virginia Department of Motor Vehicles

## Sura ya pili: Taa za barabarani, vibao na alama zilizopo barabarani

Hizi zote zinatumika kuelekeza madereva na ni muhimu kuzielewa na kuzifuata. Ni kinyume na sheria kukwepa alama hizo, kwa mfano kutembeza gari kupitia nyasi ili kukwepa taa ya barabarani.

**TAA ZA BARABARANI-** wanaotembeza magari, baiskeli, pikipiki na wanaopita kwa mguu, WOTE lazima kufuata taa za barabarani.



**Red light: Taa nyekundu**

Lazima kusimama kabisa kwenye mstari mweupe uliopo barabarani. Kama hakuna mstari mweupe, simama kabla ya kuingia kwenye junksheni (makutano)  ama kabla ya kuingia kwenye eneo ya wanaopita kwa mguu.  Simama kwenye taa nyekundu hadi ibadili rangi kuwa kijani.

<u>Kupinda kulia wakati taa ni nyekundu</u>- Unaruhusiwa kupinda kulia kama taa ni nyekundu. Kabla ya kupinda, lazima usimame kabisa, uangalie pande zote mbili kuhakikisha hakuna magari, mabaiskeli wala wanaopita kwa mguu.  Lazima uachie wenye haki kupita (yield the right-of way)

Kibao cha “NO Turn on Red” (Usipinde wakati taa ni nyekundu)

Kama kibao hicho kipo, huruhusiwa kupinda kulia. Ni lazima usubiri taa iwe kijani.

Kupinda kushoto wakati taa ni nyekundu- Ukiwa kwenye njia ya ONE WAY (magari yote yanaelekea mwelekeo mmoja) na kama unapinda kushoto kwenye njia ya ONE WAY, unaruhusiwa kupinda kushoto. Kabla ya kupinda kushoto lazima usimame kabisa, uangalie pande zote mbili kuhakikisha hakuna magari, mabaiskeli wala wanaopita kwa mguu.  Lazima uachie wenye haki kupia (yield the right-of-way).

Kama kibao cha “No Turn on Red” ipo, huruhusiwi kupinda kushoto.



**Red Arrow: Mshare mwekundu**

Inamaanisha lazima usimame kama unapenda kupinda kuelekelea kama mshare inavyoelekea. Huwezi kuendelea kama ni nyekundu.



**Flashing Red Lights- Taa nyekundu zinazowaka na kuzimika**

Simama kabisa, na achie wengine wenye haki ya kupita (yield the right of way. Unaruhusiwa kuendelea kama hakuna magari mengine, hakuna mabaiskeli wala wanaopita kwa mguu.

**Flashing Red Arrow- Mshare mwekundu unaowaka na kuzimika**

Simama kabisa, na achia wengine wenye haki ya kupita (yield the right of way). Unaruhusiwa kuendelea kama hakuna magari mengine, hakuna mabaiskeli wala watu wanaopita kwa mguu.

**Yellow light or arrow: Taa au Mshare wa Njano**  

Inamaanisha tahadhari na inatoa taarifa kwamba taa itabadili rangi. Kama hujaingia kwenye junksheni, usimame.  Kama si salama kusimama, kama umeshaanza kuingia kwenye junksheni, endelea kupita kwa mwendo taaratibu. Usiongeze mwendo kuwahi mabadiliko ya rangi ya taa.

**Flashing yellow light: Taa ya Njano inayowaka na kuzimika** 

Inamaanisha punguza mwendo na kupita taaratibu. Huwekwa kwenye eneo ambayo kuna hatari ya mabadiliko ya njia.

**Flashing yellow arrow: Mshare ya Njano unaowaka na kuzimika**

Unaruhuswa kupinda kufuata mwelekeo wa mshare kama nafasi ipo na ni salama.  Yield the right of way- achie wenye haki wapite kwanza, halafu upinde.

**Green light or arrow: Taa au Mshare wa Kijani**  

Unaruhusiwa kupita kama nafasi ipo na ni salama. Kama unapinda na magari mengine yanakuja, lazima uachie wenye haki wapite kwanza (yield the right of way). Kama taa imebadilika toka nyekundu kuja kijani na mtu yuko katikati ya barabara, yeye ana haki ya kupita, mwache apite kabla yako.

**Kama taa zote hazifanyi kazi**

Kama hakuna umeme na taa hazifanyi kazi, lazima usimame na upite kufuate utaratibu wa vibao vinne vya kusimama (four way stop) (angalia ukurasi 5) . Kama askari polisi yupo, fuata askari anavyoeleza.

**Lane Use Signals:** Taa za matumizi ya Njia- zinaeleza ni njia gani iko wazi kutumika na ipi imefungwa.



**Red X: X Nyekundu**

Njia hiyo imefungwa, usitembeza gari kwenye njia hiyo.

**Yellow X or Yellow diagonal down arrow: X ya Njano wa Mshare wanjano unaoyoelekea chini**





Njia hiyo karibu itafungwa, unatakiwa kuhama toka njia hiyo na uingie njia nyingine haraka.



**Green Arrow: Mshare ya kijani**

Njia hiyo iko wazi, unaruhusiwa kutembeza gari hapa.





**Left-turn arrow: Mshare ya kupinda kushoto (nyeupe)**

Unaruhusiwa kuingia kwenye njia yenye taa hiyo, kama utapinda kushoto kama taa inavyoonyesha.

## Traffic Signs- Vibao vya Barabarani

Rangi na muundo wa kila kibao una maana fulani. Wakati mvua inanyesha sana unaweza kuona rangi au muundo wa kibao kabla ya kusoma maandishi. Ni muhimu kuelewa rangi na muundo na maana zao.

Nyekundu- Simama, yield (achia wenye haki wapite), kukataza

Nyeusi na nyeupe- sheria za barabari


Njano- tahadhari, taarifa ya mabadiliko

Kijani na nyeupe,  Bluu na nyeupe,  kahawia na nyeupe- kutoa taarifa ya miji, majengo, maeneo ya kumbukumbu

Manjano na nyeusi, pinki na nyeusi- maeneo ya ujenzi wa barabara na lazima kupunguza mwendo

**Muundo:**

Octagon- pembe nane






Simama kabisa kwenye mstari mweupe, kwenye njia ya wanaopita kwa mguu au usawa wa kibao. Subiri magari yapite, na watu wapite kabla ya kuendelea.

Kuna junksheni zingine ni FOUR WAY STOP, kuna vibao vya kusimama kila kona. Kwenye junksheni hizo, lazima magari yote yasimame kabisa. Kama magari mawili au zaidi yanafika kwa pamoja, lazima usimame kabisa na gari lilipo mkono wako wa kulia ana haki ya kupita kwanza.


Triangle – pembe tatu






Lazima upunguze mwendo, uwe tayari kusimama.
Achie magari, mabaiskeli na wanaopita kwa mguu wapite kwanza, halafu uendelee.

Rectangle- Pembe nne ndefu, Sheria na Taarifa




Kama kibao kimesimama ina maelekezo ya sheria.



Kama kibao kimelala ina maelekezo ya taarifa.

Diamond- Pembe nne



Tahadhari, mabadiliko au hatari iko mbele

Punguza mwendo na uwe tayari kusimama .





Pentagon- Pembe tano

Eneo ya shule- zinatoa taarifa ya eneo ya wapita kwa mguu karibu na shule

**Regulatory signs- Vibao vya sheria. Lazima kufuata maelekezo ya vibao hivyo.**

Mduara mwekundu na mstari katikati unamaanisha kuna kitu kimekatazwa



Speed Limit- Mwendo wa kasi unaoruhusiwa

Kibao kinaelezea ni mwendo gani unaruhusiwa hapo wakati hali ya hewa ni nzuri. Kama kuna mvua kubwa au barafu, unashauriwa kutembeza gari mwendo chini ya kasi iliyopo kwenye kibao. Ukitembeza gari kwa mwendo uliopo kwenye kibao wakati wa mvua kubwa au wakati wa barafu, unaweza kusimamishwa na askari na kutozwa faini kwa kuwa sio mwendo salama.




Do not Enter- Wrong Way     Usiingie-  Umekosea Njia

Vibao hivyo vinaelezea huwezi kutembeza gari kwa mwelekeo huo.
Ukitembeza gari kupita vibao hivyo, unatembeza gari kinyume
na sheria na inawezekana utagongana na gari nyingine kichwa kichwa.
Tafuta sehemu kugeuzi gari lakini taratibu.







One Way- Magari yote yanaelekea mwelekeo mmoja. Magari yote lazima yapite kama mshare

unavyoonyesha.







No Left Turn: Hairuhusiwi kupinda kushoto.



No Right Turn: Hairuhusiwi kupinda kulia.



No U Turn: Hairuhusiwi kugeuza gari



No Turn on Red:  Hairuhusiwi kupinda wakati taa ni nyekundu.  Subiri taa ya kijani.





Do not Pass:  Hairuhusiwi kupita magari

Vibao hivi vinawekwa mwanzoni mwa eneo ambapo hairuhusiwi kupita magari mengine.  Huwezi kupita magari yaliyopo mbele yako hata kama nafasi ipo.





Left Turn Yield on Green- Wakati taa ni kijani unatakiwa kuachia wenye haki wapite kabla ya kupinda kushoto

Kibao hiki ni pamoja na taa za barabarani. Maana yake ni kwamba Huna haki ya kupita wakati taa ni kijani. Lazima usubiri wengine wanaokuja, wapite kwanza halafu upinde kushoto kwa uangalifu.




Keep right: Bakia kulia (bana upande wa kulia zaidi)

Mbele kuna kitu kinachogawa barabara, bakia upande wa kulia kama mshare unavyoonyesha.



Lane Use Control: Vibao hivyo vinawekwa ambapo njia ipo maalumu kwa ajili ya kupinda.  Magari yaliyopo kwenye njia hizo, lazima yafuate mwelekeo wa mshare.







High Occupancy Vehicle:  Gari linalobeba watu wengi (watu zaidi ya wawili)
Vibao hivyo vinaeleza njia maalumu kwa ajili ya magari yanayobeba watu wengi.
Magari kama basi au magari ya abiria yanaruhusiwa kutumia njia hizo, lakini si magari yenye mtu mmoja.



Disabled Parking: Eneo la kuegesha gari la wenye ulemavu
Lazima gari iwe na kibari kutoka DMV kuegesha kwenye eneo hili.




**Warning Signs- Vibao vya Tahadhari-** vinakujulisha uhusu vitu vya hatari au mabadiliko yaliyopo mbele. Punguza mwendo, tazama vibao vingine vilivyo mbele.

Advisory Speed: Mwendo unaoshauriwa kutumika

Kibao kinaeleza mwendo wa kasi unaoshauriwa na uliosalama wakati wa kutoka kwenye highway (barabara kubwa) kuingia barabara nyingine.




Reduced speed limit ahead: Mbele mwendo wa kasi unaoruhusiwa unapunguzwa

Uwe tayari kupunguza mwendo, mbele mwendo wa kasi unaoruhusiwa ni tofauti, ni mdogo zaidi




Stop Ahead/Yield Ahead: Mbele kipo kibao cha kusimama/ Mbele kipo kibao cha YIELD

Punguza mwendo, uwe tayari kusimama kwa kuwa mbele kuna kibao cha kusimama ama YIELD





Signal Ahead: Mbele ipo taa ya barabarani

Punguza mwendo, uwe tayarai kusimama kwa kuwa mbele ipo taa ya barabarani.



No passing zone: Hairuhusiwi kupita magari

Kibao kinawekwa mwanzoni wa eneo ambalo hairuhusiwi kupita magari. Huwezi kupita magari yaliyopo mbele yako hata kama nafasi ipo.



Merge: Kuungana



Njia mbili zinakuja kuungana mbele. Ni jukumu la madereva wote, wa njia zote kuhakikisha kuwa magari yanaendelea kuingia kwenye barabara moja kwa usalama.

Lane Reduction: Kupunguzwa kwa njia



Njia ya kulia inaisha mbele. Madereva waliopo njia ya kulia lazima wasogee na kuingia kwenye njia ya kushoto wakiona nafasi katikati ya magari mengine.  Madereva waliopo njia ya kushoto wanahitaji kuruhusu wengine kutoka upande wa kushoto waingie kwenje njia yao.

Divided Highway Begins: Mbele Barabara inagawanywa



Barabara inagawanyika mbele kuwa njia mbili tofauti na katikati ipo nyasi au sementi au ukuta. Kila upande ni ONE WAY, magari yanaelekea mwelekeo mmoja. Bakia kulia.

Divided Highway Ends:  Mbele Barabara iliyogawanyika inakuja kuungana tena



Kilichokuwa kinagawa barabara kama vile ukuta, nyasi au sementi itaisha. Njia zinakuja kuungana na magari yanaelekea kupanda na kushuka. Bakia kulia.



Roundabout: Kipi Lefti / Mzunguko

Kipi Lefti iko mbele. Magari yanayoingia lazima yasuburi nafasi yao kuingia, waachie wenye haki waendelee kwanza.

Slippery when wet: Panatereza panapokuwa na maji



Barabara ikiwa na maji, panatereza. Punguza mwendo. Usishike breki kwa haraka, usigeuze gari au kupinda matairi kwa haraka. Ongeza umbali kati yako na gari lililo mbele yako.

Low Clearance Sign:  Barabara inapita juu mbele na nafasi ni fupi




Mbele barabara au daraja inapita juu ya njia na nafasi ni fupi kama inavyoonyesha kwa vipimo vya futi na inchi. Usiendelee na safari kwa kutumia njia hiyo kama uko kwenye gari ndefu kwa kuwa haitapita.

Hill: Mlima



Barabara inashuka kwa kasi mbele. Jaribisha breki kama zinafanya kazi vizuri.

Deer Crossing: Eneo la wanyama pori kupita  (swala)



Kwenye eneo hili wapo wanyama pori kama swala. PUnguza mwendo, uwe macho na uwe tayari kusimama.

Pedestrian Crossing: Eneo la wapite kwa mguu





Tazama kwa wanaopita kwa mguu, punguza mwendo na uwe tayari kusimama.  Kibao ambacho kina mshare (mkuki) chini yake inaonyesha pale ambapo njia ipo kwa wapita kwa mguu.

Bicycle Crossing/ Bike Path:  Eneo la baiskeli kupita / Njia ya baiskeli





Mabaiskeli hutembea pembeni mwa magari hapa, au kupita mbele ya magari hapa. Utembeze gari kwa uangalifu.

Kibao ambacho kina mshare (mkuki) chini yake inaonyesha pale ambapo njia ipo kwa baiskeli kupita.

School Zone/School Crossing: Eneo la wanafunzi/watoto kupita





Uwe macho kwa watoto wanaopita njia. Uwe tayari kusimama, punguza mwendo. Fuata maelekezo ya askari barabarani kama anasimamisha magari kuwapatia watoto nafasi kupita. Kibao chenye mshare chini yake kinaonyesha ambapo njia ipo.

Open Joints: Ipo nafasi ya wazi au nyufa kwenye daraja




Punguza mwendo. Kwenye daraja ipo nafasi ya wazi au nyufa ambayo inaweza kumsababisha mwenye pikipiki kuanguka.

Expansion Joints: Njia ina matutamatuta




Njia ina matuta makubwa kiasi ambayo yanaweza kuangusha pikipiki, hasa wakati kuna maji barabarani.

Intersection: Junksheni (barabara zinakutana)





Junksheni iko mbele, Uwe macho kwa magari yanayokuja kuingia kwenye barabara.

Y Intersection: Junksheni kama Y



Mbele lazima uende kushoto au kulia.

T Intersection:  Junksheni kama T



Mbele njia hii inaisha. Tumia ishara (indicator/ turn signal) kabla ya kupinda kushoto au kulia.

Right Curve-Side Road: Kupinda kulia na njia ndogo toka pembeni



Mbele barabara inapinda kulia na kuna njia ndogo kutoka pembeni kushoto itakuja kuungana na barabara hiyo. Uwe macho kwa magari yanayokuja kuingia kwenye barabara hiyo.

Sharp right turn: Kipindo kikali kulia



Punguza mwendo, na uwe tayari kwa kuwa mbele barabara inapinda kikali kulia.

**Sharp** right and left turns: Vipindo **vikali** kulia na kushoto



Punguza mwendo na uwe tayari kwa kuwa mbele barabara inapinda kulia kikali, halafu kushoto kikali

Right and Left Curves: Vipindo kulia na kushoto

Mbele barabara inapinda kulia na kushoto. Punguza mwendo.



Right Curve with Safe speed indicator: Kipindo kulia na ushauri wa mwendo wa salama

Mbele barabara inapinda kulia, punguza mwendo hadi kiasi kilichoandikwa kwenye kibao, mwendo unaoshauriwa kuwa salama.




Winding Road: Barabara inapindapinda kama nyoka

mbele barabara inapindapinda kama nyoka. Punguza mwendo ili uwe na uwezo wa kudhibiti gari kizuri.



Low Ground Railroad Crossing: Njia ya reli mbele iko kwenye mwinuko

Mbele kuna mwinuko, (mlima mdogo) na njia ya reli inapita hapo. Njia ya reli inaweza kugusana na gari kwa chini kama gari iko chini sana.



Railroad crossing: Eneo la Treni kupita mbele

Mbele kuna njia ya treni kupita, uwe unatazama na unasikia kama kuna treni (gari moshi). Punguza mwendo, uwe tayari kusimama kama treni itapita.





Railroad Crossbuck: Eneo la Treni kupita

Kibao hiki kinawekwa kwenye eneo la treni kupita. Uwe unatazama, unasikia kama kuna treni. Punguza mwendo, uwe tayari kusimama. Treni inaweza kuja toka kushoto au kulia. Kama zipo njia nyingi za reli, inawezekana zaidi ya treni moja itapita hapo.




Railroad Crossbuck and Flashing lights: Eneo la Treni kupita pamoja na taa za kuwaka na kuzimika





Taa za kuwaka na kuzimika zinaweza kuwa pamoja na kibao kinachoonyesha eneo la treni kupita. Lazima usimame kama taa zinawaka na kuzimika. Usubiri hadi taa zimezimika kabisa, halafu endelea na safari.

Crossbuck, flashing lights and Gate: Eneo la Treni kupita, pamoja na taa za kuwaka na kuzimika, pamoja na geti



Geti (mbao unaoshuka na kuinuliwa kuzuia magari kupita) inatumika pamoja na taa za kuwaka na kuzimika katika eneo la treni. simama kama taa zinawaka na kuzimika kabla ya geti kushuka. Usubiri, uwe umesimama hadi taa zinazimika kabisa na geti inainuliwa juu kabisa. Usitembeze gari chini ya geti.

Alama za barabarani za X na RR, zinaweza kuwa chini kwenye barabara pia kuonyesha reli iko mbele. Hakikisha ipo nafasi ya kutosha gari lako upande wa pili wa reli kabla ya kuvuka reli.




Kumbuka, basi ya shule zitasimama kabisa kabla ya kupita kwenye reli hata kama hakuna treni.

Kibao hiki kinaeleza namba ya simu (1-800-555-5555) kama utahitaji kutoa ripoti ya hatari ya reli. Kama ni ajali utapiga simu namba 911. Kibao pia imeandikwa namba ya junksheni ya reli na barabara (#221-6200)




Kama gari lako litazimika katikati ya njia ya reli, toka nje ya gari na kukimbia.

WORK ZONE- ENEO LA MATENGENEZO YA BARABARA

Usitembeze gari kwa mwendo wa kasi zaidi ya inavyoruhusiwa kwenye eneo la matengenezo ya barabara, unaweza kupigwa faini ya $500. Kumbuka rangi ya maanjano (orange) inatumika kwenye vibao vya matengenezo ya barabara, vinatushauri punguza mwendo na uwe macho kwa mabadiliko.

Rough Road: Barabara yenye mabondemabonde




Bump: Mwinuko (tuta)


Uneven Lanes:  Njia zinapishana urefu

Njia moja ni ndefu zaidi ya njia iliyopembeni, hazina usawa





Road construction Ahead- Detour-  Matengenezo ya barabara mbele- Utapita njia tofauti

mbele barabara imefungwa na utapita njia tofauti, fuata ishara za mshare (mkuki) inavyokuelekeza. Punguza mwendo.



Flashing Arrow Panels: Vibao vikubwa vya Taa kama mishare, inawaka na kuzimika.


Inaelekeza njia ya kupita kwa kuwa mbele barabara imefungwa kwa matengenezo.




Flaggers: Wanaoshika bendera au kibao

Wafanyakazi hao wanavaa shati za njano (yellow)  au maanjano (orange). Wanatumia vibao vya STOP- simama na bendera nyekundu kuelekeza magari.

Traffic Control Devices:  Vifaa vya kudhibiti magari



mageti, madiaba, na vifaa vingine vinawekwa barabarani kuelekeza madereva njia ya kupita na wapi pamefungwa.  Tembeza gari lako katikati ya vifaa hivyo, na ufuate kibao cha mwendo unaoruhusiwa katika eneo hili.  Usibadili njia hadi umetoka kwenye eneo la matengenezo.

Slow Moving Vehicles: Magari yanayotembea kwa mwendo mdogo



Kinawekwa kwenye magari yanayotembea mwendo mdogo, 25 au chini kama vile matrekta, mikokoteni inayovutwa na farasi. Ukiona kibao hicho nyuma ya gari kama trekta, uwe tayari kupunguza mwendo sana.

PAVEMENT MARKINGS: ALAMA ZILIZOCHORWA KWENYE BARABARA

Alama zilizochorwa kwenye barabara zina rangi tofauti. Kila rangi ina maana tofauti.

Nyekundu- haitumiki sana.  Labda kuonyesha eneo ambalo haliruhusiwi kupark (kuegesha) gari.

Reflectors Nyekundu- viashiri

Zinaonyesha eneo ambalo haliruhusiwi kutembeza gari. Usiku taa za gari zikikutana na hizo, zinan’gaa sana.



Bluu- inaonyesha eneo la parking kwa walemavu.

Yellow Center lines: Mistari ya njano katikati ya barabara

zinaonyesha kuwa barabara imegawanyika sehem mbili TWO WAY-magari yanapishana, mengine yanapanda na mengine yanashuka.



Broken yellow center lines- Mstari wa njano katikati ya barabara umekatwakatwa

Kupita magari (pass) inaruhusiwa kama unapanda au kama unashuka, kama kuna nafasi kufanya hivyo.



A broken yellow line alongside a solid yellow line- Mstari wa njano umekatwakatwa uko pamoja na mstari mzima

Kupita magari inaruhusiwa kama uko upande wa mstari uliokatwakatwa. Kama uko upande wa mstari mzima, huruhusiwi kupita (pass) magari mbele yako.



Double solid yellow lines- Mistari miwili mizima ya njano

Hutenga barabara katikati kwa magari yanayopanda na kushuka. Hairuhusiwi kupita (pass) magari mengine hapo.  Huweza kupita kwenye mistari hiyo isipokuwa unapita baiskeli au unapinda kushoto.



Broken white lines- Mstari nyeupe umekatwakatwa

Hutenga barabara katikati kwa magari yanayoelekea mwelekeo moja. Unaweza kubadili njia kwa uangalifu.

Barabara nyingi hazina mistari. Kama hakuna mstari, unaruhusiwa kupita gari kama nafasi ipo na ni salama, kama hakuna kibao kinachokatazwa hivyo.

Solid white lines: Mistari myeupe mizima

Hutegenesha njia. Usibadilibadili njia kama mstari nyeupe upo kati yako na njia ya pembeni.

Mstari mweupe pia upo pembeni mwa barabara.

Mstari mweupe pia huonyesha ni wapi kusimama kabla ya kuingina kwenye junksheni.




White lane arrows are curved or straight: Mishare (mikuki) myeupe iliyopinda na iliyowima

Kama uko kwenye njia iliyochorwa mshare myeupe uliopinda na neno ONLY- ni lazima upinde kama mshare unavyoonyesha

Kama uko kwenye njia iliyochorwa mshare mweupe uliopinda pamoja na mshare uliowima, unaweza kupinda au kuendelea moja kwa moja mbele.



Double solid white lines- Mistari miwili myeupe

Hutenga magari yanayoelekea mwelekeo moja. Hasa kuonyesha HOV Lane, njia maalumu kwa magari ya abiria, yanayobeba watu zaidi ya moja. Huruhusiwi kupita mistari hiyo ama kupass.

Yield Line- mstari ya pembe tatu



Michoro ya pembe tatu kwenye barabara huonyesha eneo la YIELD- kupunguza mwendo na kuachia wenye haki kupita mbele yako. Simama kama hakuna nafasi kuingia kwenye barabara, subiri magari yote yapite.

Three lane roads- Barabara za njia tatu



Zipo michoro inayoonyesha ni wakati gani madereva wanaweza kutumia njia ya katikati kwa ajili ya kupinda au kupita magari mengine.

Kama pande zote za njia ya katikati zimechorwa na mstari wa njano mzima pamoja na mstari uliokatwakatwa- madereva wanaopanda au madereva wanaoshuka wanaweza kutumia njia ya katikati kupinda kushoto.  Njia hiyo isitumike kwa zaidi ya futi 150 (150ft).



Shared lane marking- Mchoro wa njia ya kushirikiana baiskeli na gari

Mchoro huo unatoa taarifa kwa madereva wa gari kwamba baiskeli nyingi ziko kwenye njia hiyo, watembeze gari kwa uangalifu.


Bicycle lanes- Njia maalumu ya baiskeli



Mchoro huo unaonyesha njia maalumu ya baiskeli, magari hayaruhusiwi hapo.  Kama dereva wa gari, angalia vizuri kwa kutumia kioo kabla ya kupinda kulia au kushoto kuhakikisha hakuna baiskeli pembeni.

High Occupancy Vehicles (HOV)- Magari yanayobeba watu wengi

Mchoro mweupe kama diamond kati kati ya njia unaonyesha kwamba njia hiyo ni kwa ajili ya magari yanayobeba watu wengi.






Toll Plazas and Lanes- Eneo na njia za kulipia kutumia barabara

Unapokaribia eneo la kulipia kutumia barabara, punguza mwendo, lipa kama unavyoelekeza na endelea na safari. yapo magari yanayolipa kwa utaratibu wa E-ZPass, magari hayo yameshalipia na yanapita kwenye njia maalumu yenye kibao cha E-ZPass juu. Kama hujalipia, lazima upita kwenye njia yenye kibao 'CASH' na ulipe kabla ya kuendelea na safari. Kamera zipo hapo, na usipolipa, serikali wataona namba ya gari lako kwenye picha za kamera na utapigiwa faini.



(Ken Lund, 2014)

Painted Curb: Rangi iliyopakwa pembeni mwa njia (kwenye ukuta mdogo wa njia)

| |
|---|
| **White -Nyeupe- simama muda mfupi tu, kushusha abiria au kupakia abiria** |
| **Yellow- Njano- Simama muda mfupi tu, kushusha abiria au kupakia abiria, bakia kwenye gari** |
| **Red-Nyekundu- Hairuhusiwi kusimama hapo kabisa** |
| **blue- Bluu- Kuegesha gari hapo inaruhusiwa kwa wenye ulemavu tu.** |

## Sura ya tatu- Safe Driving - Kutembeza Gari kwa usalama

Kila unapotembeza gari, unawajibika kwa matendo yako. Lazima ufuate sheria za barabara na uhakikishe usalama wako na wa abiria wako pamoja na usalama wa magari mengine barabarni.

Hand position- Mkao wa mikono

Uskani ukiwa kama saa, shika uskani kwenye namba 4 na 8 kama ilivyo kwenye picha.




Speed limits- Mwendo wa kasi unavyoruhusiwa

Mwendo wa kasi unavyoruhusiwa umeandikwa kwenye vibao. Unaweza kutembeze gari chini ya mwendo ulivyoandikwa kwenye kibao, lakini ni kinyume na sheria kutembeze gari zaidi ya mwendo ulivyoandikwa. Pia kumbuka ni lazima kutembeze gari chini ya mwendo ulivyoandikwa kwenye kibao kama uko karibu na shule, katika eneo wanapotengeneza barabara au kama hali ya hewa ni mbaya kama vile mvua kubwa au barafu.

Radar detectors ni vifaa vinavyotambua kama polisi iko karibu. Vifaa hivyo haviruhusiwi kabisa katika Virginia.

**<u>Mwendo wa kasi unaoruhusiwa:</u>**

**Interstate highway- Barabara kubwa zinazoonganisha majimbo= 55-70**

**Public highway- Barabara kubwa= 55**

**Unpaved roads- Barabara za udongo na kokoto, hazina lami= 35**

**School, business and residential areas- Barabara karibu na shule, biashara na eneo la nyumba nyingi= 25**

Kumbuka- inawezekana kuwa mwendo wa kasi ni tofauti kwenye barabara hizo, **<u>fuata maelekezo ya vibao.</u>**

Stopping- Kusimama

Lazima usimame:

- kwenye vibao vyote vya kusimama, taa zote nyekundu na taa zote zinazowaka na kuzimika nyekundu
- unapoingia kwenye njia kutoka kwenye njia ndogo kama vile toka nyumbani, unapovukwa njia ya wapita kwa mguu
- kwenye njia ya reli kama taa zinawaka na kuzimika
- unapoelekezwa kusimama na wanaotumia bendera kwenye eneo la kutengeneza barabara
- kama mtu anapita kwa mguu barabarani
- kama askari polisi anakuelekeza kusimama. Usipofuata maelekezo ya askari na kama askari anakufuata na gari lake na anauawa kwa ajali, utakuwa na kosa kubwa ya sheria- Class 4 felony.
- kama ukigonga gari au ukigongwa na gari jingine (eneo la ajali)



Stopping for school buses- Kusimama kwa basi za shule

Kwenye picha hizo, magari ya rangi nyekundu lazima yasimame, na yasubiri watoto wote wawe salama wametoka barabarani kabla ya kuendelea.

Lazima usimame kama basi imetoa kibao cha STOP na taa zinawaka na kuzimika. Pia kama basi imesimama na kibao hakipo, au taa hazipo, lazima usimame.



Si lazima kusimama kama basi imesimama kwenye upande wa pili wa barabara ilivyogawanyika.

Stopping distance- Umbali unavyotumika kwa gari kusimama

Vitu vitatu vinachangia kufanya gari lako lisimame.

1. Perception time: Muda wa kutambua hatari
   Muda unaotumika na akili yako (kichwa chako) kutambua hatari


2. Reaction time: Muda wa kutenda
   Muda unaotumika baada ya kutambua hatari na kabla ya kutenda, kabla ya kukanyaga breki

3. Braking distance: Umbali gari linatembea kabla ya kusimama

   Baada ya kukanyaga breki (kushika breki kwa nguvu), gari linatembea umbali gani kabla ya kusimama kabisa.

Hivi vitu vitatu vinakuwa tofauti kulingana na hali ya hewa, uwezo wako wa kuona, afya yako kisaikologia na afya yako kimwili. Umbali gari linatembea kabla ya kusimama pia inaathiriwa na mwendo wa gari lako, hali ya matairi na hali ya breki zenyewe. Kwa mfano barabara ikiwa na maji na ukishika breki kwa nguvu, gari litatembea kwa umbali mrefu kuliko kama barabara ingekuwa kavu.

**Kariri namba hizo kwenye picha**- inaeleza gari litatembea umbali gani kabla ya kusimama kama unatembeza gari kwa mwendo fulani wakati barabara ni kavu.



**Yielding the Right -of -Way   Kuachia wenye haki, wapite**

Yield- pia inamaanisha kusimama kama hakuna nafasi kuingia barabarani kwa usalama.

Mifano ya YIELD- kuachia wenye haki wapite

- Magari mawili yanayotoka sehemu tofauti yanafika kwenye junksheni (sehemu barabara zinakutana), gari lililotangulia kufika lina haki kupita kwanza
- Magari mawili yanayotoka sehemu tofauti yanafika kwenye junksheni kwa wakati moja, hakuna taa, gari lililopo upande wa kulia ana haki kupita kwanza
- Kama taa za barabarani hazifanyi kazi, magari yote yanayofika kwenye junksheni lazima yasimame. Dereva aliyopo kushoto anamwachie dereva aliyopo kulia apite kwanza.
- madereva wanaoingia kwenye INTERSTATE, barabara kubwa, kwa kutumia njia ya ndogo ya kuungana na barabara kubwa hiyo lazima waachie magari mengine yapite kwanza kabla ya kuungana na barabara kubwa
- Madereva wanaoingia kwenye kipi lefti (mduara) lazima waachie magari mengine yapite kwanza kabla ya kuingine kwenye kipi lefti
- Kama unatoka nyumbani kuingia njiani, lazima usimame kwanza na kusubiri nafasi kuingina njiana
- Lazima uachie wenye baiskeli na wanopita kwa mguu wapite mbele yako, hasa kama wanaotumia njia maalumu ya CROSS WALK kama punda milia.
- Wakati wa kuenda kwenye mazishi, magari mengi yanajipanga na kupita barabarani kwa pamoja. Hutangulizwa na askari polisi na huwa magari hayo yanawasha taa zao na kutembea taratibu. Huwezi kutembeza gari lako kwa kukatia kwenye maandamano hayo. Lazima usubiri magari hayo yote yapite.
- Pia kama kuna maandamano ya magari ya kijeshi- usiingie, achie wote wapite.

**Yielding to Vehicles with Flashing lights-  Kuachia magari yenye taa za kuwaka na kuzimika yapite**

Unaweza kuona magari yenye taa za kuwaka na kuzimika, rangi ya bluu, nyekundu, njano ama nyeupe barabarani.

Stopped Vehicles- magari yaliyosimama na taa za kuwaka na kuzimika

- Kama uko kwenye barabara kubwa ya njia nne, na unakaribia gari limesimama na taa zinawaka na kuzimika, jaribu kusogea kwenye njia mbali na gari hilo. Kama hakuna uwezekano kwa kusogeza gari kuingia kwenye njia mbali na gari hilo, punguza mwendo hadi 10 chini ya mwendo wa kasi unaoruhusiwa na upite kwa usalama umbali ya futi 2 toka kwenye gari. Magari hayo yenye taa za kuwaka na kuzimika ni kama vile polisi, ambulance ya hospitali, zima moto na wanaokusanya takataka au posta.

- Huruhusiwi kupark gari lako ndani ya futi 500 toka kwenye gari la zima moto (fire) kama imesimama na taa zinawaka na kuzimika

Approaching vehicles, same direction- Taa inawaka na kuzimika kwenye gari linalotembea mweleko sawasawa na wewe, gari liko mbele yako au nyuma yako

- Achie futi 500 (500ft) au zaidi kati yako na gari la zima moto, polisi, hospitali kama linatembea

na taa zinawaka na kuzimika

- Kama gari hizo zinakuja toka nyuma yako, lazima uachie barabara, wapite. Kama nafasi ipo, sogeza gari lako kulia pembeni mwa barabara na usimame hadi gari limepita.

**Roundabouts- Kipi lefti (mduarda, mzunguko**)




Kipi lefti inaweza kuwa na njia moja au mbili. Magari yanayoingia kwenye kipi lefti, lazima yasubiri na kuachie magari yaliyopo yapite kwanza. Kila njia inayokuja kuingia kwenye kipi lefti itakuwa na YIELD sign ya pembe tatu. Unaposogea karibu na kipi lefti, punguza mwendo. Tumia ishara ya indicator kuonyesha unapotaka kupita.

Kama una mpango kupinda kulia, bakia kwenye njia ya kulia kabisa.

Kama una mpango wa kunyosha, unaweza kutumia njia ya kulia au njia ya ndani.

Kama una mpango kupinda kushoto, ingia na sogea kwenye njia ya ndani.

Wakati uko ndani ya kipi lefti, bakia kwenye njia, tumia ishara ya indicator kama una mpango wa kubadili njia au kupinda. Usibadili njia bila kuangalia vizuri njia pembeni mwako kama kuna magari yanayozidi kuzunguka pembeni mwako.




**Changing Lanes= Kubadili Njia**

Kabla ya kubadili njia, 1- angalia vyoo nje ya gari na ndani inayoonyesha nyuma kuchuguza magari yaliyopo nyuma yako. 2- Halafu washa ishara ya indicator kuonyesha una mpango kubadili njia.
3- Angalia kwa haraka juu ya bega lako kuangalia kama kuna magari kwenye eneo kipofu (blind spot).

*Eneo kipofu (blind spot)* ni eneo pembeni mwa gari lako, karibu na mlango wa nyuma ambapo halionekani vizuri kwa kutumia kioo cha nje wala kioo ya kuangalia nyuma. Ni muhimu sana kuangalia eneo hili kabla ya kubadili njia, kwa kuwa gari linaweza kujificha hapo, na ukisogea pembeni, mtagongana.

Kama unabadili njia, unapita (pass) gari nyingine, unaingia au kutoka kwenye barabara kubwa, lazima kuwasha ishara ya indicator pamoja na kuangalia magari yaliyopo nyuma na pembeni mwa gari lako.

Passing - kupita magari




Wakati unapita gari jingine:

*angalia magari yaliyo mbele, nyuma na kwenye eneo kipofu kabla ya kupita gari. Tumia ishara ya indicator halafu ongeza mwendo kidogo kupita gari. Rudi kwenye njia ya kulia unapoona gari ulilolipita kwenye kioo cha nyuma.

*Huruhusiwi kupita gari kwa kuenda mwendo mkubwa kuliko mwendo unaoruhusiwa kwenye eneo hilo

*ni lazima kupita gari kabla ya kuingia kwenye NO PASSING ZONE, eneo lisiloruhusu kupita magari. Ukiwa unapita gari na unaona kibao cha NO PASSING ZONE, umevunja sheria.

*unaruhusiwa kupita kwenye mkono wa kulia kama gari unalolipita limewasha indicator kupinda kushoto. Huruhusiwa kupita mkono wa kulia kwenye nyasi au nje ya barabarani.

*unapopita baiskeli au pikipiki yenye mwendo mdogo kama moped, punguza mwendo na upite ukiacha nafasi ya futi 3 au zaidi kati yako na baiskeli.

Muhimu- kama gari linakupita wewe, usiongeza mwendo. Endelea na mwendo uliopo au punguza mwendo kidogo.

Kupita magari ni kinyume na sheria na si salama:

- kwenye mwinuko, milima, barabara zenye vipindo, kwenye eneo barabara zinakutana, na eneo la reli isipokuwa kama barabara ina njia mbili au zaidi yanayoelekea pamoja
- pembeni mwa barabara kwenye nyasi, nje ya barabara
- wakati basi imesimama kushusha au kuchukua watoto
- wakati mstari katikati ya barabara ni mzima upande wako wa barabara

**Overcorrecting-** Kurekebisha zaidi (kurekebisha uskani kupita kiasi)

Overcorrecting inatokea wakati dereva anapindisha uskani kikali zaidi ya alivyotarajia. Dereva akipindisha uskani sana, matairi ya nyuma yanatereza nje ya barabara. Dereva anaweza ashindwe kudhibiti gari.

Ajali zinazosababishwa na overcorrecting huwa ni ajali ya gari moja, ajali hizo zinaweza kuzuiliwa. Kama dereva, punguza mwendo kama barabara inapindapinda. Kwa bahati mbaya, ukitoka nje ya barabara, usichanganyikiwe- unatakiwa kupunguza mweendo, angalia ni wapi unatakiwa kutembeza gari na rudisha gari taratibu barabarani.

**Turning- kupinda**

**Ili kupinda kulia:** uwe kwenye njia pembeni mwa barabara, upande wa kulia kabisa. Washa indicator/ishara sekunde 3 au 4, au futi 100 kabla ya sehemu kupinda. Tazama kushoto kama watu wanapita kwa mguu au wako na baiskeli au kuna magari mengine. Shika breki taratibu, halafu pindisha gari.

Unapopinda kulia kuingia kwenye barabara ya njia nyingi, unaingia kwenye njia iliyopo kulia zaidi.

**Ili kupinda kushoto**: uwe kwenye njia iliyopo kushoto zaidi, na uingie kwenye njia iliyopo kushoto zaidi. Unafuata alama zilizopobarabarani au kwenye vibao, wakati mwingine njia zaidi ya moja inapinda kushoto. Washa indicator/ishara sekunde 3 au 4, au futi 100 kabla ya sehemu kupinda. Tazama kushoto kama watu wanapita kwa mguu au wako na baiskeli au kuna magari mengine. Shika breki taratibu, halafu pindisha gari.

Kabla ya kupinda- hakikisha matairi yanaelekea moja kwa moja hadi utakapokuwa tayari kupindisha gari. Hii inazuia gari lako kusukumwa kuingia kwenye njia ya magari kama utagongwa kutoka nyuma. Wakati nafasi ipo ya kupinda kushoto, pindisha gari taratibu.

Kama magari mawili yanaangaliana, na yote mawili yamewasha ishara kupinda kushoto, magari yatapinda kushoto mbele ya mwenzake ili pande za abiria zinapishana. (Angalia picha hapo)



**U-Turns Kugeuza gari**



Kugeuza gari barabarani hairuhusiwi kila sehemu. Kabla ya kugeuza gari, hakikisha hakuna kibao kinachokataza U-turn au kinachokataza kupinda kushoto. Katika eneo la biashara nyingi, kugeuza gari hairuhusiwi. Kugeuza gari hairuhusiwi kwenye highway- barabara kubwa.

Kama utageuza gari, washa ishara ya kupinda kushoto, simama, achia magari wenye haki kupita mbele yako. Kama nafasi ipo, endelea kugeuza gari ukiingia kwenye njia iliyopo kulia kabisa.

**Turn Signals- Ishara za kupinda (indicator)**

Ukihitaji kubadili njia, kupinda au kuingia/kutoka kwenye barabara lazima utumie ishara ya gari. Washa indicator/ishara sekunde 3 au 4, au futi 100 kabla ya sehemu kupinda. Ukimaliza kupinda au kubadili njia, zima ishara.

Kama ishara haifanyi kazi, unaweza kutumia ishara za mikono kama hapo kwenye picha.



| | | |
|---|---|---|
| Left turn | Right turn | Slow or Stop |
| Kupinda kushoto | Kupinda kulia | Kupunguza/Kusimama |

**Maintaining a Space Cushion- Achia nafasi kati yako na magari mengine**

Nafasi kati yako na magari mengine inakupatia muda zaidi kutambua hatari, kushika breki na kuepuka ajali. Achia nafasi kati yako na magari mengine kwa kutembeza gari katikati ya njia yako. Hakikisha nafasi ipo kati yako na gari lililopo mbele yako, pia nafasi kati yako na gari lilipo nyuma yako ili kupishana kwa usalama.

Tumia sheria ya sekunde 2,3, 4 kujua kama umeacha nafasi ya kutosha kati yako na gari lililopo mbele yako.

| Following Distance- Umbali toka gari lako na gari mbele yako | |
|---|---|
| Sekunde 2 | Chini ya mweendo wa 35mph |
| Sekunde 3 | Mweendo wa 35mph- 45mph |
| Sekunde 4 | Mweendo wa 45mph – 70mph |

- Angalia gari mbele yako inapopita kibao au mti
- Anza kuhesabu sekunde hadi utakapopita kibao hicho
- Ukifika kwenye kibao ndani ya sekunde mbili kama unatembeza gari mweendo chini ya 35, uko karibu zaidi na gari hilo. Unatakiwa uwe mbali zaidi, punguza mweendo kuachia nafasi kubwa zaidi kati yako na gari hilo.
- Kama hali ya hewa ni mbaya, kama magari ni mengi au kama barabara ni mbaya, ongeza umbali kati yako na gari lililopo mbele yako.






Pia ongeza umbali kati yako na gari lililopo mbele yako wakati:

- uko nyuma ya gari kubwa na huwezi kuona vizuri mbele yake
- hali ya hewa ni mbaya au kuna magari mengi
- wakati wa kutoka kwenye barabara kubwa kama interstate kuingia barabara ya kawaida
- uko nyuma ya baiskeli au pikipiki
- kama gari linakufuata kwa karibu sana nyuma (anakula mkia)

**Tailgating - kula mkia**

Gari linapokufuata kwa karibu sana nyuma anakula mkia wako. Usishike breki kwa nguvu. Unaweza kushika breki kidogo kuwasha taa za breki na kupunguza mweendo kidogo ili kumwambia gari lililopo nyuma akupite.

**Searching-kutafutatafuta kwa macho**

Kutafuta kwa macho ni kutazama na kuangaza barabara na kuepuka kuangalia kitu kimoja kwa muda mrefu. Tumia macho kuangalia barabara na mazingira yaliyopo karibu na barabara ili kutambua hatari zilizopo karibu.

Tazama mbele- madereva wataalamu huangalia sekunde 20 au 30 mbele ili kutambua kibao, taa za barabara, magari na wanaopita kwa mguu. Angalia kwa magari yanayopinda mbele yako.

**Kabla ya kuingia kwenye intersection/ sehemu barabara zinapokutana-** tazama vizuri pande zote mbili kabla ya kupita. Angalia kushoto kwanza, halafu kulia, halafu kushoto tena kabla ya kupita.

**Look behind- Tazama nyuma**

Tumia kioo cha kuangalia nyuma kutazama magari yaliyopo nyuma kila baada ya sekunde 10. Utaweza kuona kama gari inakuja kwa mweendo wa kasi kutoka nyuma au kama gari linakula mkia wako. Tazama magari ya nyuma kama unabadili njia, kama unarudisha gari nyuma, kama unashika breki kwa nguvu au kama unashuka kwenye mlima mkali.

**blind spots MAENEO KIPOFU**

Maeneo kipofu ni maeneo ya hatari, maeneo yasiyoonekana kwenye vyoo vya pembeni au kioo cha nyuma. Unaweza kuona maeneo hayo vizuri kwa kuangalia juu ya bega lako kwa haraka. Ni lazima kufanya hivyo kabla ya kubadili njia au kabla ya kupita gari jingine.

Epuka kutembeza gari lako kwenye eneo kipofu la gari jingine.

**Sharing the road- Kushirikiana kutumia barabara**

Madereva ya magari wanashirikiana kutumia barabara na wanaopita kwa mguu, wanaotumia baiskeli, pikipiki , mabasi na wengine.

**Pedestrians-Wanaopita kwa mguu**

- Uwe mwangalifu katika eneo la shule, eneo la michezo na kwenye nyumba nyingi kuangalia watoto wanapopita njiani
- Angalia pia kwa wazee wanapopita kwa mguu, wanaweza wasione au kusikia vizuri
- Angalia sana wakati unapinda kulia au kushota. Wanaopita kwa mguu wana haki ya kupita mbele yako kama unapindisha gari.

Baiskeli- baiskeli wana haki kama gari na wanatakiwa kufuata alama na taa zote kama magari. Wenye baiskeli ana haki kutembeza baiskeli katikati ya barabara kama anapinda kushoto au kama barabara ni nyembamba sana. Sheria ya Virginia inasema-<u>magari lazima yaachie nafasi ya futi 3 kati ya gari na baiskeli.</u>

**Mopeds: Pikipiki ndogo**

Ni kinyume na sheria kutembeza pikipiki ndogo zaidi ya 35mph. Dereva wa pikipiki ndogo lazima awe na miaka 16 au zaidi, na kutumia kofia. Huwezi kutembeza pikipiki ndogo kama umenyan'ganywa leseni ya udereva.

**Pikipiki-**

Karibia nusu ya ajali za pikipiki zinazosababisha kifoo, zinakuwa kati ya pikipiki na gari. Mara nyingi, mwenye gari anashindwa kuona pikipiki.

- Tazama kuona pikipiki. Ni ndogo na wakati mwingine vigumu kuona pikipiki
- angalia kwenye maeneo kipofu, hakikisha hakuna pikipiki pembeni mwa gari kama unabadili njia au unapinda kushoto.
- Usitembeza gari karibu na pikipiki kwa nyuma (kula mkia). Achia nafasi kubwa kati yako na pikipiki. Kama hali ya hewa ni mbaya, acha nafasi mara mbili.
- Achia upana wa njia yote kwa ajili ya pikipiki. Usitembeze gari pembeni mwa pikipiki kwenye njia moja. Yeye ana haki ya njia kama gari jingine.
- Achia pikipiki apite mbele yako kama ni haki yake kufanya hivyo, sawa na magari mengine.

**Low speed vehicles**

Magari yenye mweendo ndogo yana haki kupita kwenye barabara za kawaida kama dereva ana leseni na gari liko na registration (Usajiri wa) serikali. Unawaachia nafasi kama baiskeli na kuwaheshimu vilevile.


**Lori, Magari makubwa ya mizigo, Mabasi na magari nyumba (RV)**

Magari hayo ni makubwa, marefu na mazito zaidi ya gari la kawaida. Wanatumia umbali mkubwa zaidi kusimama. Pia kuna eneo la hatari kwenye magari hayo ambapo ni rahisi kupata ajali. Maeneo hayo yanaitwa NO-ZONES.

No-Zones zipo pembeni, mbele na nyuma ya magari makubwa na ni kama maeneo kipofu. Gari ndogo likitembea kwenye eneo hilo, dereva wa gari kubwa haweza kuona gari dogo.

**Side No-Zones**

Pembeni mwa magari makubwa yapo No-Zones kubwa, kwa kuwa magari hayo lazima yatumie eneo kubwa la barabara kupinda kushoto au kulia. Kama uko pembeni mwa gari kubwa na huwezi kuona dereva kwenye kioo chake cha pembeni, yeye hakuoni vilevile.



**Rear No-Zones**

Nyuma ya magari makubwa pia kuna No-Zones. Ukiwa karibu na gari kubwa kwa nyuma, yeye hakuoni na wewe huwezi kuona mbele yake. Achia nafasi kubwa kati yako na gari kubwa.

**Front No-Zones**

Mbele ya magari makubwa pia kuna No-Zones. Ukiwa mbele ya gari kubwa kwa karibu, dereva hakuoni. Anaweza kukugonga kwa nyuma. Ukipita gari kubwa, hakikisha unaona gari yote vizuri kwenye kioo cha nyuma kabla ya kurudi mbele yake. Usipunguze mwendo kwa ghafla mbele ya gari kubwa, magari hayo yanahitaji muda wa kutosha kupunguza mweendo.

**Wide Turns**- Kutumia eneo kubwa kupinda

Magari makubwa yanatumia eneo kubwa ya barabara kupinda. Madereva wa magari makubwa hawaoni kama gari ndogo ipo karibu pembeni kwenye eneo kipofu, futi 20 pembeni au futi 200 nyuma.

## Light to Medium Trailers:  Mikokoteni inayovutwa na gari ndogo

Mikokoteni hiyo inaunganishwa na gari kwa kutumia minyororo pamoja na kiungo maalum (hitch). Kama gari ndogo inavuta mkokoteni, ni vyema gari liwe na vioo vikubwa pande zote mbili ili kuona vizuri hadi nyuma ya mkokoteni.  Wakati wa kuvuta mkokoteni, gari linakuwa na mzigo mkubwa zaidi kwa hiyo gari litatumia muda mrefu zaidi kuongeza mweendo kupita magari, kusimama au kupinda.



Kabla ya kutembeza gari lenye mkokoteni

- hakikisha kiungo maalum (hitch) imeshika vizuri kwa kutumia pini
- hakikisha minyororo imeunganishwa vizuri kati ya gari na mkokoteni
- hakikisha nyaya za taa zimeunganishwa vizuri kati ya gari na mkokoteni
- Hakikisha taa za breki na alama za kupinda (indicator), pamoja na taa za kumulika liseni zote zinafanya kazi kwenye mkokoteni




Wakati unatembeza gari lenye mkokoteni

- achia nafasi kubwa kati yako na magari mengine wakati unabadili njia ama kupita magari
- mkokoteni ukianza kuvuta pande moja wa barabara, elekeza uskani wa gari unapotaka kuenda (usipindishe pindishe uskani)
- wakati wa kurudisha gari nyuma- kama huona vizuri, omba mtu mwingine asimame nyuma kukueleza. Kupindisha mkokoteni kushoto, tumia mkono wa kushoto. Kupindisha mkokoteni kulia, tumia mkono wa kulia.

### Backing- Kurudisha gari nyuma

Madereva wengi wanafanya kosa kubwa wanaporudi nyuma- wanashindwa kuangalia pande zote mbili nyuma ya gari. Vioo havionyeshi eneo lote la nyuma. Kuona eneo kubwa zaidi, geuka kulia na angalia nyuma. Rudisha gari taratibu, angalia kwa wanaopita kwa mguu au magari. Angaza pande zote mbili nyuma ya gari.

### Parking- Kuegesha gari

Unapoegesha gari pembeni mwa barabara, egesha gari mbali na eneo linapopita magari. Ukiegesha kwenye nyasi, egesha mbali na barabara. Ukiwa mjini, egesha karibu sana na ukuta mdogo (curb) pembeni mwa barabara. Egesha gari upande wa kulia wa barabara.


Kama barabara ni ONE WAY (ya mwelekeo mmoja), unaruhusiwa kuegesha gari upande wo wote.

<u>Kuegesha kwenye mlima:</u>

With a curb: kama ukuta mdogo upo

Kama unaegesha gari lako pembeni mwa barabara yenye ukuta mdogo, kwenye mteremko (kushuka mlima), pindisha matairi ya mbele **kulia**. Hii itazuia gari kusogea kuingia barabarani breki zikiachia.


Kama unaegesha gari lako pembeni mwa barabara yenye ukuta mdogo, kwenye mpando (kupanda mlima), pindisha matairi ya mbele **kushoto**. Hii itazuia gari kusogea kuingia barabarani breki zikiachia.



Without a curb: kama hakuna ukuta mdogo

Kama unaegesha gari lako pembeni mwa barabara na hakuna ukuta mdogo, upo kwenye mteremko (kushuka mlima), pindisha matairi ya mbele **kulia**.  Hii itazuia gari kusogea kuingia barabarani breki zikiachia.

Kama unaegesha gari lako pembeni mwa barabara na hakuna ukuta mdogo, kwenye mpando (kupanda mlima), pindisha matairi ya mbele **kulia**. Hii itazuia gari kusogea kuingina barabara breki zikiachia.




Huruhusiwi kuegesha gari (imekatazwa):

- pembeni mwa gari jingine barabarani
- kwenye eneo la kupita kwa mguu (punda milia) au njia ya kupita kwa mguu (side walk)
- mwanzo wa njia za kuingia kwenye nyumba
- eneo ambapo kuna rangi ya njano au nyekundu kwenye ukuta mdogo (curb)
- eneo ambapo kuna kibao cha NO PARKING
- eneo la parking ya walemavu
- barabarani
- ndani ya futi 15 toka kifaa cha maji kwa zima moto
- ndani ya futi 20 toka intersection- eneo la barabara mbili kukutana
- kwenye njia ya baiskeli
- ndani ya futi 15 toka njia kuingia stasheni ya emergency au zita moto
- ndani ya futi 500 toka magari ya emergency au zima moto wakati magari hayo yamewasha taa
- ndani ya futi 50 toka njia ya reli

## **Visibility**- Uonekano (uwezo wa kuona)

Kitu kinachochangia zaidi kuleta ajali ni kwa dereva kushindwa kutambua/ kushindwa kuona hatari. Wakati wa kutembeza gari, lazima unaangalia pembeni mwa barabara, barabara kwa mbele na hata nyuma wa gari lako.

Lights- Taa za gari

Sheria ya Virginia inalazimisha madereva kuwasha taa za gari wakati wa hali ya hewa mbaya kama mvua, mawingu mazito, na barafu kama uonekano wa mbele ni mdogo kama futi 500 tu. Pia ni lazima kuwasha taa za gari kama umewasha WINDSHIELD WIPERS.

Hazardous conditions- Hali ya Hatari

Kutembeza gari inakuwa hatari wakati uonekano (uwezo wa kuona) umepungua au wakati barabara ina maji ama barafu.  Lazima kupunguza mwendo.  Ongeza umbali kati yako na magari mengine mara 2 zaidi.

Night Driving- Kutembeza gari wakati wa usiku

sunset- Wakati jua linaanza kuzama, washa taa za gari. tumia taa za gari kuanzia wakati huo hadi jua linapochomoza asubuhi.

Tumia taa ndogo (low beam) ukiwa mjini.  Kama uko kwenye mitaa ambayo haina taa, unaweza kutumia taa kubwa (high beam) lakini ukikutana na gari jingine, lazima ubadili na kuweka taa ndogo. Kama unafuata gari nyingine, ukimkaribia ndani ya futi 200, tumia taa ndogo.

Tumia taa kubwa (high beam) ukiwa kwenye barabara kubwa. Lakini kama gari liko mbele anakuja na ni futi 500 mbele, weka taa ndogo.  Kama gari jingine linakuja na limeweka taa kubwa, epuka kuangalia kwenye taa moja kwa moja, angalia pembeni mwa barabara.  Usiweke taa kubwa kama yeye ameweka taa kubwa, inaumiza macho.

Fog- mawingu mazito (ukungu)

Mawingu mazito yanaweza kurudisha mwanga toka kwenye taa kukurudia machoni.  Tumia taa ndogo kama kuna mawingu mazito.

Rain- Mvua

Wakati wa mvua kubwa ni hatari hasa kama upepo unapuliza sana. Tumia taa ndogo ili uone na uonekane. Tumia WIPERS. Mvua inapoanza kunyesha, ndani ya nusu saa ya kwanza ni hatari zaidi kwa kuwa maji yanachangayika na mafuta barabarani na kuleta hatari ya kuteleza.

Snow-Barafu (ice)/theluji (snow)

Ondoa barafu na theluji yote toka kwenye gari lako kabla ya kutembeza gari. Ondoa toka juu ya gari, nyuma, na juu ya injini. Barafu na theluji ikibaki kwenye gari, ukitembeza gari, vipande vinaweza kutoka na kurushwa kwa gari jingine na kuleta hatari barabarani.

Hakikisha umetoa barafu kwenye vioo vyote na taa za mbele na nyuma pia.

Ukiweka matairi ya “all weather” yanayotumika wakati wa hali ya hewa yoyote, inasaidia matairi yasiteleza kwenye barafu.

Kutembeza gari kwenye theluji ngumu ni kama kutembeza gari kwenye barafu. Unaposhika breki, shika kwa taratibu. Punguza mweendo taratibu. Angalia darajani na maeneo ya kivuli kwa barafu. Daraja ni rahisi kuwa na barafu kuliko barabara ya kawaida.

## Dangerous Driving Behaviors- Tabia za madereva hatari

### Aggressive driving- Kutembeza gari kwa hasira

Tabia hii ya kutembeza gari kwa hasira ni kuchokoza, kuumiza au kuzuia mtu mwingine wakati wa kufanya kosa moja au zaidi ya udereva. Mifano ni:

*kushindwa kusimama kwenye kibao cha STOP

* kuepuka kifaa cha kudhibiti magari barabari kama vile vilivyopo kwenye eneo la matengenezo ya barabara

* kushindwa kuacha gari likupite

Wakati madereva hawa wanatembeza gari, wanakuwa wa hatari kwa kuwa wanaonyesha hasira zao kwa madereva wengine. Wanavunja sheria kwa kutosimama kwenye taa nyekundu, wanaenda mweendo wa juu, wanakula mkia wa magari mengine, wanapita magari upande wa kulia sio kushoto. Wanaweza kuonyesha ishara mbaya kwa mikono au usoni.

Jilinde! Ukiona dereva kama huyo, epukana naye. Usijaribu kumpita. Epuka kumwangalia machoni. Usimwangalie.

Kama unahukumiwa na kosa la kutembeza gari kwa hasira- unaweza kunyima leseni kwa siku 10 hati miezi 6.

### Distracted driving- Kutembeza gari na vipoteza mawazo (vuruga mawazo)

Kutembeza gari kunahitaji akili yako yote. Kuna vitu vingi vinaweza kupoteza mawazo yako barabarani kama vile: kubadili redio, kuongea na abiria, kuangalia maduka nje, kula chakula, kutumia simu n.k. Barabarani, madereva wasitumie simu, kompyuta au vifaa vingine vya umeme isipokuwa kutoa taarifa ya ajali polisi- 911. Kama unahitaji kufanya hivyo, egesha gari pembeni mwa barabara.

Sheria ya Virginia inazuia madereva chini ya miaka 18 kutumia simu wakati wanatembeza gari. Kuandika sms/text au kusoma sms/text ni marufuku kwa madereva wote.

Kila mwaka, vipoteza mawazo vinasababisha asilimia 20 ya ajali hapa Virginia. Vipoteza mawazo vinatoa mawazo ya dereva kutoka kwenye kazi ya udereva na wanaanza kufikiria juu ya mambo mengine. Dereva anashindwa kutambua hatari haraka na anashindwa kutenda kulingana na hatari, kisha anapata ajali. Madereva vijana na wale wasio na mazoezi ya kutosha kutembeza gari wanapoteza mawazo haraka zaidi.

Epuka hatari hizo kwa kufanya yafuatayo:

- Uwe makini. Elekeza akili na macho kwenye kazi ya udereva tu. Kaa wima kwenye kiti, elekeza macho unapoelekea na sio pembeni.
- Weka redio au muziki unapotaka kabla ya kuanza kutembeza gari.
- Usitumie simu
- Angalia magari, barabara na mazingira ya mbele kujua kinachokuja. Pia angalia vioo mara kwa mara kujua hali inayokuzunguka
- Achia nafasi na kutosha kati yako na gari mbele yako.

## Drowsy Driving- Kutembeza gari unasinzia (wakati wa usingizi)

Kupiga miayo, macho mazito, kutoona vizuri kibao, kuingia kidogo pembeni mwa barabara zote ni dalili za kuwa na usingizi wakati wa kutembeza gari. Hali hii ni hatari kupata ajali, na kufanya uamuzi mbaya wakati wa kutembeza gari. Unashindwa kuwa makini kama una usingizi.

Kuepuka kutembeza gari na hali yausingizi:

*Lala masaa ya kutosha kabla ya kuanza safari

*Epuka kutumia pombe au chakula kingi, kizito kabla ya kutembeza gari

*epuka madawa yanayoweza kuathiri uwezo wako wa kutembeza gari

*epuka kutembeza gari kwa masaa mengi. Tembeza masaa 2, pumzika, tembeza tena

*simama eneo salama na lala kwenye gari kama ni lazima. Hata dk 20 inaweza kusaidia

*tembeza gari na dereva mwingine kama unaenda safari ndefu, mnaweza kupokezana kazi ya udereva

*Epuka kutembeza gari kuanzia saa 4.00 usiku hadi saa 12.00 asubuhi. (10pm to 6am)

Kushusha kioo, kutafuna jojo, kuweka sauti kubwa ya musiki, kutumia kahawa,soda au dawa zingine za caffeine si njia nzuri kuwa macho barabarani.

Ukiona dereva anasinzia barabarani, toa taarifa kwa polisi.

## Drinking and Driving - Utumiaji wa pombe na kutembeza gari

Kisheria- mtu mwenye umri wa miaka 21 au zaidi akitembeza gari na kipimo cha pombe/kileo mwilini inaonekana kuwa asilimia .08 au zaidi anatembeza gari amelewa (DUI). Ukitembeza gari kimakosa na kipimo kinakuwa chini ya asilimia .08, baado unaweza kuhukumiwa kwa kosa la kutembeza gari umelewa. Kama dereva ana umri chini ya miaka 21 na kipimo kinaonesha asimilia .02 hadi .08, anaweza kuhukumiwa kwa kosa la kutumia kileo kinyume na sheria. Vile vile, kama asilimia ni zaidi ya .08, anaweza kuhukumiwa kwa kosa la kutembeza gari amelewa (DUI). Kama uwezo wako wa kutembeza gari umeathiriwa na madawa au kileo kingine tofauti na pombe, unaweza kushitakiwa na kuhukumiwa kwa makosa ya DUI.

Kuanzia saa 4.00 usiku na saa 8.00, madereva 3 kati ya 10 barabarani wamelewa. Karibia asilimia 50, au nusu, ya madereva wanashitakiwa na kosa la DUI wanasema wanatumia pombe kidogo tu, wakiwa na marafiki. Katika maisha yako, kuna uwezekano 50/50 kuwa utakuwa kwenye ajali inayosababishwa na utumiaji wa pombe.

Pombe na vileo vinaathiri uwezo wetu wa kuona, kuamua na uhusiano kati ya akili na misuli ya mwili.

Ounce (kipimo cha majimaji) Ounce 12 za bia ina kileo sawa sawa na kiroba cha konyagi au kileo kikali, ni sawa sawa na ounce 5 za divai.

Kupunguza kileo mwilini, kahawa, maji baridi au mazoezi hazitasaidia. Muda wa masaa ndio itapunguza kileo mwilini.

Magari yanapogongana kwa sababu ya pombe, si ajali kwa sababu yanaweza kuzuiliwa.

Unapoenda kwenye sherehe au sehemu watu wanatumia pombe kwa pamoja, amua mapema ni nani hatatumia pombe ili awe dereva salama.

Mtu akichanganya pombe na madawa ya kulevya huongeza hatari. Kama unatumia madawa ya mafua halafu unapata bia moja, inaweza kuathiri akili yako kama umetumia bia nyingi.

Kuna madawa mengi yanayouzwa dukani, yanaweza kuleta hali kama kulewa na kusinzia. Soma maelezo ya madawa kabla ya kutumia.

## Traffic crashes- Ajali za magari

Kama umepata ajali (kama umegonga gari au kama umegongwa), lazima ufanya hayo:

- simama kwenye eneo la ajali au karibu na eneo la ajali bila kuzuia magari mengine kupita. Labda utatoa magari barabarani kidogo kabla ya polisi kufika kama magari yanazuia magari mengine.
- toa msaada unavyoweza kama mtu ameumia. Usitoe mtu kwenye gari kama ameumia.
- Toa ripoti kwa polisi haraka iwezekanavyo. Ajali zote zinazoleta uharibifu wa mali, pamoja na ajali zinazosababisha mtu kuumia lazima ripoti itolewe kwa polisi.
- badilishana taarifa kwa wanaohusika kwenye ajali
    - jina, anuani na namba ya liseni ya udereva kwa madereva wote
    - namba ya leseni ya gari ya magari yote
    - jina na anuani ya watu wote waliojehuriwa
    - jina na anuani ya wote walioshuhudia ajali
    - jina na anuani na namba ya insurance ya magari kwa madereva wote

* Pia toa taarifa kwa insurance ya gari lako haraka.

Polisi watatoa ripoti ya ajali kwa ofisi ya DMV (kitengo cha magari ya Virginia) kama imesababisha mtu kuumia, kifo au uharibifu wa mali zaidi ya $1500. Taarifa hiyo itakuwa kwenye rekodi ya madereva waliopata ajali hiyo.

Ukigonga gari na mwenye gari hayupo, lazima ujaribu kumtafuta. Kama hayupo, acha karatasi ya maelezo, majina yako, namba ya simu, tarehe na muda wa ajali pamoja na maelezo ya uharibifu uliotokea. Pia lazima kutoa ripoti polisi ndani ya masaa 24.

## Deer hazards- Hatari ya wanyama pori (Swala)

Maelfu ya ajali yanatokea kila mwaka Virginia kwa sababu ya swala. Ili kuepuka kugonga swala fanya yafuatayo:

- Uwe makini zaidi wakati jua linazama na linachomoza, hasa wakati kipindi cha baridi inaanza
- Punguza mweendo unapoona swala karibu na barabara au anavuka barabara. Swala hutembea kwenye makundi, ukiona moja, wengine wako karibu.
- Usipige kengele kuwashitua.
- Kama unafikiri utagonga swala, usijaribu kukwepa swala kwa kuingia kwenye njia nyingine. Bakia kwenye njia yako, shika breki kwa nguvu na simama.

Ukigonga swala, toa ripoti kwa polisi.

## Traffic stops: Kusimamishwa na polisi

Ukisimamishwa na polisi fanya ifuatayo:

- Tulia kwanza
- Egesha gari lako pembeni mwa barabara kwenye sehemu salama
- Washa taa nne zinazowaka na kuzimika (flashers)
- Kama ni usiku, washa taa za ndani ya gari
- Zima injini, redio au muziki
- Shusha kioo upande wa dereva ili kuongea na askari polisi
- Usitoe mkanda wa usalama, pia abiria wasitoe mikanda yao
- Bakia kwenye gari, usitoke. Utatoka tu kama polisi ataomba ufanye hivyo
- Weka mikono yako sehemu ya wazi, mikono ionekane vizuri kwa polisi wakati wote

Pia omba abiria waweke mikono yao sehemu ya wazi, wasifiche mikono.

- Usiruke au kushituka pande yoyote, polisi anaweza kufikiri unajaribu kuficha kitu
- Siku zote, Ubebe ID kama leseni ya udereva, pamoja na registration (usajiri wa) gari, na dhibitisho ya insurance. Kama polisi ataomba kuona hizo, mwambia ziko wapi halafu anza kuzitoa taratibu ukiacha mkono mmoja umeshikilia uskani.
- Kama polisi anatembeza gari ambalo halina alama ya polisi au kama hana mavazi ya polisi, unaweza kumwomba kitambulisho/ID yake.
- Jibu maswali yake vizuri na kwa maelezo ya kutosha. Kama una mtazamo tofauti ya polisi, usijadili hapo, utapata nafasi kuelezea mtazamo wako ukiwa mahakamani.
- Polisi ataomba uweke saini kwenye citation. Kutia saini hapo si kukubali kosa. Kutia saini ni kukubali kwamba umeelezewa kosa kwa upande wa polisi. Ukikataa kusaini, unaweza kuwekwa jela au kupelewa kituo cha polisi.

# Sura ya 4: Mikanda ya usalama, mifuko ya hewa na viti vya watoto

## Seat Belts: Mikanda ya usalama

Katika Virginia, dereva na abiria wote kwenye kiti cha mbele, lazima wavae mikanda ya usalama. Dereva lazima ahakikishe kuwa abiria wote chini ya miaka 18, wamevaa mikanda vizuri. Na ni jukumu la dereva kuhakikisha watoto wako kwenye viti vinavyowafaa.

Lazima kuvaa mkanda ukiwa unapita juu ya bega na kuvuka kifua mbele. Usiweke mkanda nyuma wa mwili wako. Wajawazito (pregnant women) wavae mikanda pia, mkanda wa chini upita chini ya utumbo.

## Airbags: Mifuko ya hewa

Mifuko ya hewa hutoka wakati ya ajali kama gari litagonga kitu mbele. Mifuko ya hewa huweka miito kati ya watu wanaokaa mbele na sehemu ya mbele ya gari katika ajali. Kama gari lako lina mifuko ya hewa (airbags):

- tumia mikanda ya usalama pamoja na abiria wote
- Weka kiti cha udereva ili kifua chako kiwe inch 10 toka uskani
- Kama uskani unaweza kurekebishwa kuenda juu/chini, elekeza uskani chini kidogo ili mfuko wa hewa uelekee kifuani na sio kichwani
- watoto wenye miaka 12 au chini ya hapo, wavae mikanda na wakae nyuma

## Child Safety Seats: Viti vya usalama kwa watoto

Mtoto akiwekwa kwenye kiti cha usalama kwenye gari kinaweza kupunguza hatari ya kuumia au hatari ya kifo kama kuna ajali.

Watoto wote chini ya miaka minane (8) lazima wakalie viti vya usalama kwenye gari. Watoto chini ya miaka miwili (2) wakae kwenye viti vinavyoangalia nyuma ya gari na kwenye kiti cha nyuma. Kama gari halina kiti nyuma, kiti hicho kinaweza kuwekwa kiti cha mbele na mifuko ya hewa imezimwa.

Ni jukumu la dereva kuhakikisha watoto wamekaa kwenye viti vinavyowafaa. Kosa la kwanza ni faini ya $50, kosa ya pili au zaidi ni faini ya $500 au zaidi.

Sifa za mtoto ambaye anaweza kukaa bila kiti cha usalama:

- Mkanda unabana vizuri juu ya mapaja/miguu
- Mkanda wa bega, unapita kwenye bega na mbele ya kifua
- ni mrefu kutosha kukaa bila kujikunja mbele
- magoti yanafikia mwisho wa kiti cha kawaida cha gari
- anaweza kuegemea nyuma vizuri

Kama mtoto anashindwa kukaa kwenye kiti cha usalama kwa sababu ya kiafya, lazima awe na maeleza na 'waiver' toka kwa daktari.

Wakati  watoto wapo kwenye gari:

- sehemu salama zaidi mtoto kukaa ni katikati ya kiti cha nyuma
- kuna vituo vingi vinavyotoa huduma kuangalia viti vya watoto na kutoa ushauri bure
- Usibebe mtoto kwa kumshikilia na mikono yako, ukiwa kwenye ajali mikono yako itaachia na mtoto anaweza kuumia vibaya kwa kukandamizwa kati ya mwili yako na kiti au mlango.
- hakikisha milango ya gari imefungwa. Usiruhusu watoto kuchezea milango ya gari au kufuri.
- usibebe watoto nyuma kwenye nafasi ya mizigo
- ni kinyume na sheria kubeba mtoto chini ya miaka 16  kwenye gari la wazi nyuma.

# Sura 5: Penalties - Adhabu

Ukivunja sheria baadhi tena na tena, haki yako ya kutembeza gari inaweza kuwa suspended-sitishwa kwa muda, au inaweza kuwa revoked-ondolewa kupitia mahakama au ofisi ya DMV.

Suspension- inamaanisha haki imesitishwa kwa muda. Wakati mwingine unalipa faini kupata leseni tena. Pia unahitaji kuonyesha dhibitisho kuwa unaishi katika Virginia. Kama leseni yako itaexpire/itaishia muda wake, lazima ufanye mitihani tena ya kuandika na kutembeza gari.

Revoke- inamaanisha haki imeondolewa. Ili kupata liseni tena, lazima uombe leseni, ufanye mitihani yote tena na ulipe faini zinazokuhusu.

## Conviction-related suspensions and revocations: Leseni kusitishwa au kuondolewa kwa sababu ya kuhukumiwa na makosa ya sheria

Mahakama au ofisi ya DMV wanaweza kusitisha au kuondoa leseni yako kwa makosa yafuatayo:

- kutembeza gari wakati umelewa DUI
- kuumiza mtu wakati unatembeza gari na umelewa
- kutembeza gari wakati leseni imesitishwa/imeondolewa kwa kosa la DUI
- kutembeza gari ambalo linakosa ignisheni (kifaa cha kuwasha injini)
- kutoa maelezo ya uongo ofisi ya DMV
- kushindwa kusimama kwenye eneo la ajali na kujitambulisha kama mtu ameumia au amefariki kwenye ajali
- kosa la mauaji kutokana na ajali ya gari (kosa la makusudi au si makusudi)
- kosa la mauaji, si makusudi, wakati umelewa na unatembeza gari
- kosa lo lote la madawa ya kulevya hata kama si wakati wa kutembeza gari
- kosa lengine kisheria kwa kutumia gari (mfano ni kuiba kwa kutumia gari)
- kufanya mtihani wa udereva kwa niaba ya mtu mwingine
- kusema uongo kwa polisi, kuepuka polisi barabarani

Mahakama inaweza kusitisha au kuondoa leseni kama utahukumiwa na makosa hayo:

- kutembeza gari kwa hasira
- kutembeza gari bila leseni
- kutembeza gari wakati leseni yako imesitishwa au kuondolewa kwa kosa la DUI
- kukataa kupima pumzi (hewa) au damu wakati umeshitakiwa na kosa la DUI
- kushindwa kulipa mafuta kwenye kituo cha mafuta

Ukihukumiwa na kosa lo lote la kawaida ndogo barabarani, na umeshindwa kulipa faini ndani ya siku 30, mahakama watasitishwa leseni yako.

## Maelezo mengine ya kusitishwa na kuondolewa kwa liseni

### Driver improvement program- Darasa la kuboresha udereva

Ofisi ya DMV (kitengo cha magari hapa Virginia) wana jukumu la kutunza rekodi za madereva wote pamoja na makosa yao kisheria. Ukiwa na makosa kisheria kwenye rekodi yako, DMV inakupatia points. DMV inaangalia umepata points ngapi ndani ya mwaka, na ndani ya miaka 2.

Chini ya miaka 18: Ukihukumiwa na kosa la udereva, ofisi ya DMV watakulazimisha kusoma darasa la kuboresha udereva. Usipomaliza darasa ndani ya siku 90, DMV watasitisha leseni hadi utakapomaliza darasa.

Ukifanya kosa la pili, na uko chini ya miaka 18, leseni itasitishwa kwa siku 90. Kwa kosa la tatu, leseni itaondolewa kwa mwaka mzima au hadi utakapofika miaka 18.

Zaidi ya miaka 18: DMV itakulazimisha kusoma darasa la kuboresha udereva kama una points 12 ndani ya mwaka moja (miezi 12), au kama una points 18 ndani ya miaka 2 (miezi 24). Usipomaliza darasa ndani ya siku 90, DMV wataondoa leseni.

Ukipata zaidi ya points 18 ndani ya mwaka moja (miezi 12) au points 24 ndani ya miaka 2, (miezi 24) DMV watasitisha leseni kwa siku 90 na pia lazima kusome darasa la udereva.

### Medical review program- Utaratibu wa kuhakikisha afya

DMV ina jukumu kuhakikisha madereva wote wana afya nzuri kutembeza gari kwa usalama.

DMV ikipata taarifa kuwa dereva ana afya mbaya, wanaweza kuomba dereva huyo apate ripoti toka daktari kudhibitisha hali yake ni nzuri kutembeza gari. Pia wanaweza kuomba dereva arudia mitihani.

Hali ya afya husika ni:

*kuzimia/ kupoteza fahamu

*uwezo wa kuona

*uwezo wa kuamua

*uwezo wa misuli kufanya kazi

Insurance Monitoring Program- Utaratibu wa kufuatilia insurance

DMV ina jukumu kuhakikisha wenye magari wana kuwa na registration (usajiri) ya magari yao. Unapo-register gari, (unaposajiri gari) lazima utoe udhibitisho ya kuwa na insurance ya gari au kunasaini maelezo kuwa hauna insurance na utalipa $500 kama faini ya kukosa insurance.

Ofisi ya DMV itasitisha leseni kama:

- utashindwa kudhibitisha una insurance
- insurance ya gari inaisha muda na unashindwa kuleta namba za gari kwa ofisi ya DMV

Suspensions for failing to satisfy child support related requirements- Leseni kusitishwa kwa kosa la kushindwa kutoa matumizi ya watoto

Kitengo cha kuhakikisha matumizi ya watoto kinaweza kutoa ripoti DMV kusitisha haki ya udereva kama:

- umechelewa kutoa malipo ya matumizi ya watoto kwa siku 90 au $5000
- umeshindwa kufika mahakamani ulipoitwa kwa kesi ya kutoa matunzo/matumizi ya mtoto

Alcohol and the law: Pombe na sheria

Ukishikwa na kuhukumiwa na kosa la kutembeza gari umelewa, adhabu ni kubwa. Polisi akifikiri umelewa, ataomba ufanye kipimo cha hewa au damu kuangalia kiasi cha pombe kwenye mwili. Kama unatembeza gari barabarani, tayari umekubali kufanya kipimo hicho kama polisi ataomba ufanye hivyo. Kama ukipata ajali na polisi anajua ni kwa sababu ya pombe, unaweza kushikwa kwa kosa la DUI ndani ya masaa 3, bila hati ya mahakama.

Ukikataa kufanya kipimo cha hewa au ukifanya kipimo na kiasi ya kileo (BAC) kwenye mwili ni .08 au zaidi, polisi atakushitaki na kosa la DUI. Leseni itasitishwa hapo hapo. Kwa kosa la kwanza, leseni itasitishwa siku 7. Kwa kosa la pili, itasitishwa siku 60 au utakapoenda mahakamani. Kwa kosa la tatu, itasitishwa hadi utakapoenda mahakamani.

Mahakamani ukihukumiwa na kosa la DUI, wanaweza kusitisha au kuondoa leseni au kutoa faini.

Kumbuka- ukisimamishwa na polisi, akiona chupa ya pombe wazi kwenye gari au ukionyesha dalili za kutumia pombe, polisi anaweza kukushitaki.

Ukikutwa na kosa la DUI na una abiria chini ya miaka 17 kwenye gari, utalala siku 5 jela, pamoja na faini na adhabu zingine husika. Unaweza kutozwa faini zaidi $500 au $1000, pamoja na kulazimishwa kufanya kazi za jamii kwa masaa 80.

Gari kuchukuliwa

Ukikutwa unatembeza gari baada ya kusitishwa leseni kwa kosa la DUI, gari lako litachukuliwa kwa siku 30 .  Ukikutwa unatembeza gari baada ya kusitishwa leseni kwa kosa jingine, pia gari litachukuliwa kwa muda, hadi utakapopata leseni tena au siku 3.

Restitution- Kulipa

Kulingana na sheria za mji, unaweza kulazimishwa kulipa sehemu ya gharama za huduma za 911 emergency kama zima moto, na magari ya hospitali kama utasababisha ajali kwa kosa la DUI.

Makosa mengine yanahusu pombe kwa watu chini ya miaka 21

Kama uko chini ya miaka 21 na unatembeza gari na kiasi ya pombe kwenye mwili ni .02 hadi .08, umetumia pombe kinyume na sheria. Mahakamani wanaweza kutoa adhabu hizo:

- kusitisha leseni kwa mwaka moja
- kutoza faini $500
- kukulazimisha kufanya kazi za jamii masaa 50 au zaidi

Ukikutwa kiasi ya pombe kwenye mwili ni zaidi ya .08- utashitakiwa kama mtu mzima na kupata adhabu hizo zilizoelezwa hapo juu.

Ukimpatia mtu chini ya miaka 21 pombe, au ukimpatia mtu aliyelewa pombe zaidi, unaweza kutozwa faini $2500, leseni kusitishwa kwa hadi mwaka moja au unaweza kulala jela mwaka moja.

Ukiwa chini ya miaka 21 na ukitumia ID feki kununua pombe, unaweza kupatwa na adhabu hizi:

- faini $500
- Kulazimishwa kufanya kazi za jamii 50
- kulala jela hadi miezi 12
- kusitishwa leseni kwa miezi 6 hadi mwaka moja